

ELIMU INAYOMLENGA MTOTO (IEP) MASHAURI KWA WAZAZI

TATHMINI

Kutoa Rufaa na Kuomba Tathmini ya Mwanzo:

- ✓ Omba kwa tathmini kwa maandishi; weka nakala ya ombi lako.
- ✓ Elezea matatizo ya mtoto na sababu ya tathmini inahitajika.
- ✓ Idhini ya mzazi inahitajika kwa tathmini.
- ✓ Wazazi wana haki ya kupata Tathmini Huru ya Elimu ya mwanafunzi kama hawakubaliani na tathmini ya shule.

Maswali ya Kuuliza Kuhusu Tathmini:

- ✓ Tathmini inapima nini?
- ✓ Alama ya wastani au kawaida katika mtihani huu ni gani?
- ✓ Mtoto wangu yuko kiwango gani kwa kulinganisha na kawaida?
- ✓ Hii inamaanisha nini katika kumfunza mtoto wangu?

SIFA ZINAZOHITAJIKA

- ✓ Inakitwa katika tathmini na maoni ya timu ya IEP.
- ✓ Lazima mwanafunzi awe katika moja ya viwango aina 13 na ahitaji mafunzo maalumu.
(Tazama kijitabu cha IEP kwa maelezo zaidi.)

MATAYARISHO KWA AJILI YA MKUTANO WA IEP

Matayarisho ya Mkutano wa IEP:

- ✓ Kusanya habari ya kushiriki: kiafya, kisaikolojia, tathmini nyinginezo.
 - Weka faili ya habari zote muhimu zinazohusiana na rekodi ya masomo ya mtoto wako.
 - Hakiki rekodi ya masomo ya mtoto wako na IEP ya sasa ya mtoto wako kama ipo.
- ✓ Orodhesha unachoona kama uwezo na mahitaji ya mtoto wako.
- ✓ Andika chini mambo ya kupewa kipaumbele na malengo ya muda mrefu kwa mtoto wako.
- ✓ Orodhesha huduma ambazo unaamini mtoto wako anahitaji ili kufikia malengo uliyoyatambua.
- ✓ Andika chini maswali yako.

- ✓ Wasiliana na timu yako kabla ya mkutano:
 - Omba na uhakiki takwimu za tathmini.
 - Shiriki fikira zako kuhusu malengo ya IEP na timu yako.
 - Omba nakala ya mswada wa malengo ya IEP kabla ya mkutano wa timu.

Alika Watu kwenye Mkutano wa IEP:

- ✓ Wazazi wanaweza kualika yeyote wanayeamini atakuwa wa msaada katika mkutano wa IEP.
- ✓ Wape habari kuhusu uliyemwalika kuja kwenye mkutano wa IEP kabla ya mkutano.
- ✓ Wanafunzi wanahimizwa kushiriki katika mkutano wa IEP mahali panafaa.
- ✓ Wanachama muhimu katika Timu ya IEP: Mzazi(wazazi), LEA (Local Education Agency), Mwalimu wa Elimu Maalumu, Mwalimu wa Elimu ya Jumla.

MATAYARISHO KWENYE MKUTANO WA IEP

- ✓ Tumia ujuzi mwema wa mawasiliano kipindi chote cha mkutano.
- ✓ Mwakilishi wa LEA ndiye anafaa kuongoza mkutano.
- ✓ Wacha wanachama wa IEP wajitambulisha na majukumu yao.
- ✓ Lazima wazazi wapewe nakala ya Ilani ya Utaratibu wa Kinga ya Utah inayoelezea haki za mzazi maalumu chini ya IDEA.
- ✓ Hakikisha mashaka kuhusu mtoto wako na uwezo wake vimeorodheshwa kwenye IPE.
- ✓ Elezea mambo unayotaka yapewe kipaumbele na malengo yako. Fikiria jinsi yatakavyoingiliana na malengo yapendekezwayo na wengine kwenye timu.
- ✓ Jitayarishe kushauriana. Ona kama kuna njia mbadala za kufikia malengo.
- ✓ Omba ufafanuzi wa habari yoyote au kauli zisizokuwa bayana kwako.

Maana ya Sahihi Yako:

- ✓ Washiriki wote wanafaa kusaini IEP.
 - Sahihi zote kwenye IEP huonyesha walioshiriki na waliohudhuria.
 - Wazazi wanaweza kuandika kwenye IEP kwamba “hawakubaliani” au wana mashaka.

KUFUATILIA MKUTANO WA IEP

- ✓ Elezea shukrani zako kwa juhudi za wataalamu wa shule.
- ✓ Fuatilia maendeleo ya mtoto wako.
 - Fahamu ni mara ngapi ripoti ya maendeleo itatumwa nyumbani na fahamu njia bora ya kuwasiliana na wengine wa timu ya IEP.
- ✓ IEP inaweza kugeuzwa kulingana na hitaji.
 - Wazazi wanaweza kuomba mkutano wa IEP kama kuna mashaka au matatizo na IEP au kama mtoto hapigi hatua za kuridhisha.

✓ Timu za IEP zinafaa kukutana mara moja kwa mwaka.

UTATUJAJI WA MATATIZO KATIKA MCHAKATO WA IEP

Endelea kwa umakinifu! Jaribu kusuluhisha ugumu katika kiwango cha chini iwezekanavyo.

Kukitokea Ugumu:

- ✓ Wasiliana na timu yako ya shuleni.
- ✓ Fuatilia itifaki ya amri ambayo kawaida ni:
 1. Mwalimu
 2. Mwalimu Mkuu
 3. Mkuu/Mkurugenzi wa Wilaya wa Elimu Maalumu
 4. Ofisi ya Elimu ya Jimbo la Utah, Elimu Maalumu.

Vifungu Vyote vya Sheria ya Elimu kwa Watu wenye Ulemavu (IDEA 2004) pia vinatumika katika Charter Schools.

Kwa taarifa ya kina angalia kijitabu cha “Parents as Partners in the IEP Process” katika Utah Parent Center

www.utahparentcenter.org/publications/handbooks



Utah Parent Center